

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU (Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu Na. +255 028 2810339
Fax Na. +255 028 2810339
E-Mail/Baruapep:ded@kasuludc.go.tz
Website:www.kasuludc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),
S. L. P 97,
Kasulu — Kigoma,
TANZANIA.

Kumb.Na. **KSDC/S.2/19 VOL.II/12**

20/12/2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu anawatangazia Watanzania wenye sifa kutuma maombi kwa ajili ya kujaza nafasi za kazi zenye **masharti ya Mkataba wa mwaka mmoja** zifuatazo:-

1. Msaidizi wa Hesabu – **Accounts Assistant (NAFASI 2).**

A: Sifa za muombaji.

- Kuajiriwa aliyehitimu elimu ya kidato cha 4 au 6 mwenye Astashahada (**Cheti – NTA LEVEL 5**) katika fani ya Uhasibu kutoka chuo/taasisi yoyote inayotambuliwa na serikali.
- Kuajiriwa wenye cheti cha ATECH Level II au “Foundation level” kinachotolewa na NBAA.

B) Kazi za kufanya/majukumu.

- i) Kuandika na kutunza rejesta zinazohusu shughuli za uhasibu,
- ii) Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya Fedha,
- iii) Kutunza majalada yenye Kumbukumbu za Hesabu,
- iv) Kupeleka barua au nyaraka za uhasibu Benki.
- v) Kufanya usuluhisho wa masurufu, karadha, hesabu za benki na Amana.

c) MSHAHARA – TGS.B (390,000).


D) MASHARTI KWA UJUMLA KWA WAOMBAJI.


- Waombaji wawe ni raia wa Tanzania wasiozidi umri wa miaka 45.
- Waomba waambatishe Wasifu (CV) ya hivi karibuni ikiwa na mawasiliano, anuani ya posta, barua pepe, na namba za simu zinazopatikana.

- Waombaji mnapaswa kuambatisha vivuli vya vyeti vifuatavyo: Astashahada, ATECH II, kidato cha VI/IV, cheti cha kuzaliwa.
- Barua ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza kwa unadhifu na kuambatisha picha ndogo (**passport 1**).
- Mwombaji kazi ambaye ni Mtumishi/Mwajiriwa atatakiwa kupitisha barua yake ya maombi kwa mwajiri wake wa sasa.
- Waombaji wataokidhi vigezo ndio wataoitwa kwa ajili ya usaili.
- Hati za matokeo (result slips), Testimonials havitakubalika.
- **Barua zote zitumwe kwa njia ya Posta tu kwa anuani ifuatayo:-**

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 97,
KASULU

- Mwisho wa kupokea maombi yote ni tarehe **04.01.2019** siku ya **Jumatatu** saa **9:30** alasili.


Eng. Godfrey M. Kasekenya,
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
KASULU



NB:

Tangazo hili linapatikana kwenye mbao zote za matangazo na kwenye wavuti ya Halmashauri (www.kasuludc.go.tz)